## FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL1

## KISWAHILI PAPER 3 ANSWERS

# SEHEMU YA A (Alama 20 )

### KIDAGAA KIMEMWOZEA - Ken Walibora

1. (a) (i) Maneno ya Ben Bella.

(ii) Akimwambia Mashaka mpenziye.

(iii) Kupitia kwa barua aliyomwandikia kueleza ameutamatisha uhusiano wao.
(iv) Babake Mashaka alikuwa na usuhuba na Lowela dadake Ben Bella. Ben Bella anasema kauli hii kutokana na uovu wa babake mashaka ambao ameufichua kwa Mashaka (4x1=al.4)

(b) (i) Msemo- alaa kuhihali-kwa vyovyote vile –maovu yanayotendeka hayawezi kuzuilika.

(ii) Chuku - Dunia kupasuka ufa mkubwa - Kuonyesha uzito wa maovu ambayo yatatendeka duniani.

(iii) Jazanda/Isitiara-Dunia kuwa na ufa, Jamii kupotoka kimaadili.(zozote 2x2=4) Kutaja -1 Kueleza -1
(c) (i) Wananchi wananyang'anywa mashamba yao k.m -mamake Imani –shamba la Baraka Chirchir Hamadi.
(ii) Wanafunzi kushiriki mapenzi na walimu wao-k.m Fao anamringa mwanafunzi wake.

(iii) Wahariri kutoa na kuichapisha miswada kwa majina yao-k.m Mwalimu Majisifu aliiba Mswada wa Imani.
(iv) Wazazi kupuuza malezi ya wanao k.m Mwalimu Majisifu kwa watoto wake walemavu.

(v) Wauguzi kupuuza wajibu wao k.m wauguzi walikataa kukitibu kitoto uhuru.

(vi) Askari kutesa raia-k.m Amani na Imani walipigwa na askari wakiwa ndani ya seli.

(vii) Walimu walevi kutelekeza jukumu la kufundisha wanafunzi-k.m Mwalimu Majisifu hafiki kazini.

(ix) Viongozi katili kuendelea kushikilia nyadhifa za viongozi km Mtemi Nasaba Bora.

(x) Watoto walemavu kudhalilishwa na wazazi wao k.m Dora anawaficha watoto wake mlango unapobishwa.
(xi) Ukatili wa askari –k.m kumpiga mamake Imani Kitutu.

(xii) Wazazi kutupa watoto wao wachanga k.m Lowela na Mtemi walimtupa mtoto mlangoni pa Amani.
Hoja za kwanza 6 za mwanafunzi 6x2=12 –kutaja-1 -Kueleza-1

# SEHEMU YA B (Alama 20 )

### TAMTHILIA MSTAHIKI MEYA -Timothy M. Arege

2. 2)(i) Katili –haoni tatizo la mtoto mmoja kufa.

(ii) Mapuuza –Hazingatii malalamishi ya wafanyikazi.

(iii)Ubinafsi

–kuagiza maji yake pekee
-Kujilimbikizia mali.

-Kula vyakula vingi

(iv) Tamaa ya mali-wizi wa fimbo.

-Unyakuzi wa viwanja.

(v) Dhalimu-kutuma polisi kupiga watu.

(vi) Mauaji –vifo vya awali vya waandamaji.

(vii) Fisadi –kisa cha mwanakandaras
(viii) Laghai/mwongo-kudanganya kuwa dawa zipo njiani.

(ix) Unafiki-kujidai mcha Mungu.
(x) Ubaguzi

-kuongoza madiwani mishahara.

-Kuajiri mhazili asiyehitimu. Zozote 5x2=10 Kutaja -1 Kueleza-1

**SIKI**

(i) Mtetezi wa haki-aliwasilisha malalamika ya wafanyakazi kwa Meya.

(ii) Mwajibikaji –kila mara yuko hospitalini kuwahudumia wagonjwa.

(iii)Mshauri mwema-anawashauri Diwani III, Meya na viongozi wa wafanyakazi.

(iv) Mzalendo chanya-Haungi mkono sera mbovu za Meya hata kama ni nduguye.

-Haungi mkono Sera za kigeni za mipango ya milenia.

(v) Msimamo dhabiti-Hayumbishwi na vitisho vya Meya.

(vi) Jasiri –Anamkosoa Meya bila hofu.

(vii) Mwenye huruma

-Ni mwenye utu.

-Anawashughulikia wagonjwa licha ya hali ngumu hospitalini Zozote 5x2=10 Kutaja -1 Kueleza-1

3. (a)(i) Haya ni maneno ya Tatu

(ii) Akimwambia Meya.

(iii)Walikuwa ofisini mwa Meya.

(iv)Tatu pamoja na wawakilishi wengine wa wafanyikazi walikuwa na mkutano na Meya kuwasilisha malalamiko ya wafanyikazi

(b) Msemewa ni Meya.

(i) Meya hashughuliki masilahi ya wafanyikazi.

(ii) Mishahara ya wafanyikazi kucheleweshwa.

(iii)Wafanyikazi wanalipwa mishahara nusunusu.

(iv) Mishahara ya wafanyikazi ni ya chini.

(v) Gharama ya maisha imepanda. (vi) Watoto wa wafanyikazi wanafukuzwa shuleni kwa ukosefu wa karo.

(vii) Hakuna dawa hospitalini.

(viii) Wafanyikazi wana maisha duni-Huishi mabandani na kutembea kwa miguu jua likiwaka.

(ix) Wafanyikazi wanashindwa kugharamia matibabu.

(x) Wanafanya kazi katika mazingira duni-kukosa glavu za kuosha vyoo.

(xi) Watoto wanakufa kutokana na njaa na magonjwa-mtoto wa kerekecha.

(xii) Wananyikazi kutomudu chakula bora kula sukumawiki na dona.(zozote 4x2=8)

(c) (i) Migomo ya wafanyikazi.

(ii) Uchafu mjini Cheneo.

(iii) Kuahirishwa kwa safari ya wageni waliotarajiwa.

(iv) Kuzorota kwa maendeleo –maji kusombwa kwa punda.

(v)Vifo vya watu.

(vi)Mkurupuko wa magonjwa –k.m kipindupindu.

(vii)Kuzorota kwa viwango vya elimu.

(viii)Kuzorota kwa huduma za afya.

(ix)Kupoteza nafasi ya uongozi –k.m Meya. (zozote 4x2=8)

## SEHEMU YA C (Alama 20 )

### USHAIRI

3. 4. (a)

(i) Tathlitha-mishororo mitatu kila ubeti.

(ii)Kikwamba-Neno El-nino limetumiwa kuanzia kila mshororo.

(iii)Bantudi-lina vipande vinne kwa kila mshororo.
(iv) Ukara –vina vya mwisho vinatiririka ilhali vya kati vinabadilikabadilika. (4x1=al.4) Kutaja -½ Kueleza-½

(b) (i) Kuharibu makazi.

(ii) Mkurupuko wa magonjwa.

(iii)Kufilisisha watu.

(iv) Kuzorota kwa miji.

(v) Huleta hofu/majonzi/wasiwasi.

(vi) Unyevunyevu kila mahali/kutota. (zozote 4x1=al.4)

(c)(i) Tabdila –Nafusi –badala ya nafsi. -Ujako- badala ya ujapo

(ii) Inkisari –twambwa –badala ya twambiwa.

-Latajwa –badala la linatajwa.

-Uma –badala ya umma.

-Taleta-badala ya utaleta.

(iii) Kuboronga sarufi-Wewe na vyako vikosi badala ya –wewe na vikosi vyako.

-Mno hutupa kusota-hutupa kusota mno.

-Mbawa zipate kuota –badala ya zipate kuota mbawa. Zozote 2x2=al.4 Kutaja-1 Mfano-1

(d) (i) Lina beti sita.

(ii) Kila ubeti una mishororo mitatu.

(iii) Vipande vine katika kila mshororo.

(iv) Vina vya mwisho na vyaq ukwapi vinatiririka.

(v)Mpangilio wa mizani ni 3-8-5-8 isipokuwa ubeti wa 3-mshororo wa pili na ubeti wa 5- mshororo wa kwanza. Zozote 4x1=4

(e)(i)Tashhisi-harufuyo yatughasi. -Tangazo lako.

(ii)Jazanda/Isitiara-unyasi. -Nyoka. 2x1=al.2 Kutaja -½Mfano-½

(f) Wakati wengi wanaleta madhara ya el-nino kuna wachache wanaonufaika. al.1x2=al.2 5.

5)(a) (i) Muundo wa beti haulingani.

(ii) Idadi ya mishororo inatofautiana.

(iii) Hakuna urari wa vina.

(iv) Idadi ya mizani ni tofauti.

(v) Migao katika mishororo hailingani. (zozote 4x1=al.4)

(b)(i) Hushughulikia wakimbizi.

(ii) Hutoa magari ya ambulensi.

(iii)Hutoa huduma za kiafya.

(iv)Hufika haraka kwenye mikasa.

(v) Hutoa huduma za dharura. (zozote 3x1=3)

(c) Mshairi anaanza kwa kusema kuwa anamvulia kofia na kumpa jina la msimbo.Anasema anampa heshima na kumwita awaza kama zao la wazawa.Anamshukuru kwa kufika kwenye majanga na kutenda hisani.Anatamatisha kwa kumwambia kuwa kufa ndio kufaana. (al.3)

| (e) | Kaka (serikali) | Shirika |
|---|---|---|
| (i) | Huchelewa kuchukua hatua. | -Huchukua hatua haraka. |
| (ii) | Hukosa vifaa muhimu. | -Wana vifaa vingi k.m magari. |
| (iii) | Analaumiwa ka utepetevu. | -Anapongezwa kwa ari na bidii. |

(d)(i) Msemo-vulia kofia.

(ii)Tashhisi-Nakubatiza.

-Pigia saluti.

-Nakuita awaza. (2x1=al.2) Kutaja-½ Mfano-½

(f)(i)Tunu-zawadi/tuzo/pongezi.

(ii) Jamala-wema/Hisani/ukarimu/furaha. (2x1=al.2)

## SEHEMU YA D (Alama 20 )

### HADITHI FUPI DAMU NYEUSI

4. 6. (i) Ubaguzi wa rangi-Fikirini alibaguliwa.

(ii) Wizi wa kimabavu-Fiona na Bob.

(iii)Unyanyasaji kutoka kwa polisi,majaji weupe na magereza

(iv) Mapenzi ya kiholela-Fiona kujipendekeza kwa Fikirini

(v) Umiliki wa silaha haramu-Bob. (zozote 3x2=6)

MWANA WA DARUBINI

(i) Wanawake kunyimwa fursa ya kusoma

(ii) Ajira ya watoto.

(iii)Ulevi- Mwatela.

(iv) Ubakaji-Kananda kubakwa na Mwatela.

(v) Kunyang'anywa mtoto-mtoto wa Kananda kuchukuliwa na Mwatela.

(vi) Kuozwa kwa lazima-Kananda aliuzwa kwa mkongo kama mke. (zozote 3x2=6)

SHAKA YA MAMBO

(i) Utapeli-Kamata kumtapeli Esther kwa kusema kuwa atamfikishia mzungu pesa.
(ii) Kukosa uaminifu-Kamata hakuwa rafiki wa dhati wa Esther.Alionekana kuwa na mpango wa kando na Grace. (2x2=al.4)

TAZAMANA NA MAUTI

(i) Tamaa –Lucy alitamani kuishi uingereza na alikuwa tayari kutumia njia yoyote - haramu au halali.
(ii) Unafiki –Lucy hakumpenda mzungu Crusoe bali alipenda mali na kuishi London.
-Tena alitamani mzungu afe ili arithi. (2x2=al.4)

7. (a)(i)Maneno ya Msoi.

(ii) Alikuwa akizungumza na mpenzi Asha.

(iii) Walikuwa wameenda kujistarehesha kama desturi.Usiku ule Msoi alionekana mwenye mawazo mengi na hakuwa na furaha.Asha alimrai Msoi ale. (4x1=al.4)

(b)(i)Tashbihi/Tashbiha-kama kupe.

(ii) Swali balagha-usemi huu ni swali lisilohitajika jibu. (2x2=4 Kutaja-1 Mfano-1

(c)(I)Mzungumzaji ni Msoi.

(i) Ana Imani ya kishirikina-aliamini ndoto na ishara maishani mwake na aliziona kama utabiri wa mambo yajayo.

(ii) Mwoga-anaogopa vizuu.

(iii) Mwenye bidii-alifanya kazi kwa bidii wiki nzima.

(iv) Mpenda raha na burudani-anapenda Exotic Resort kujiburudisha kila wikendi.

(v) Mchezaji dansi hodari-siku ile hakucheza kwa usogora wake wa kila siku.

(vi) Hana msimamo-anashawishika kwa haraka- anashawishiwa na Semkwa na anakubali kwenda baa ya makaburini. (3x1=al.3)

(d)(i)Msoi anataka kujikinga na mashetani.

(ii) Msoi aliota ndoto na kuziamini kuwa za kweli.

(iii) Kwa Msoi kujikwaa mlangoni na bakuli lake la maua kuvunjika ni ishara mbaya.

(iv) Msoi kujibana kidole akifunga mlango wa gari ni shara mbaya

(v) Mimwesho na ngurumo za radi njiani zinambabaisha Msoi.

(vi) Msoi aliamini wafu watafufuka kwa sababu wamechoka kukerwa na kelele za walevi hotelini.

(vii) Kutoweka kwa nyota na mwezi ni ishara ya mambo mabaya kutendeka usiku ule. (3x2=al.6)

## SEHEMU YA E (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI

5. 8. (a)(I)Ni sherehe au ada za kitamaduni zinazoonyesha usanii wa maonyesho ya kuiga jinsi matukio Fulani yalivyofanyika katika uhalisia wa maisha

au

–Ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalum cha mwaka. (al.2)

(II)(i)Jando na unyago-kufunza nasaha na maadili.

(ii)Matanga –kuwaliwaza waliofiwa.

(iii) Vita –kuomba ushindi kabla ya vita na kushukuru baada ya vita.

(iv) Kuzaliwa kwa mtoto-kumpa mtoto jina.

(v) Arusi-kuwapongeza maarusi.

(vi) Matambiko-kutoa shukrani na kuomba.

(vii)Mavuno-kutoa shukrani kwa mungu.

(viii) Kutambua mashujaa-kuwatukuza na kuwahongera.
(ix) Kuwatawaza viongozi-kuwapongeza viongozi waliochaguliwa. (zozote 3x2=al.6) Kutaja-1 Maelezo-1

(b) (i) Hulenga jamii maalumu tu.

(ii) Ujumbe hueleweka tu na jamii husika.

(iii)Huweza kujumulisha baadhi ya maudhui na hivyo huweza kukanganya.

(iv) Ujumbe hauwezi kupitishwa kwa siri.

(v) Huhitaji ufundi maalum wa kimanaa-hupigwa na watu teule tu-hivyo huwa tatizo kutokeapo dharura na sogora mwenyewe asipatikane.

vi)Haiwezi kufaa katika masafa marefu.

(vii)Watoto huenda wasipate ujumbe kwa njia inayofaa. (zozote 6x1=6)

(c)(i)Kufanya utafiti kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi.

(ii)Kufundisha fasihi simulizi shuleni.

(iii)Kuhimiza kuandikwa au kuwepo kwa vitabu vya Fasihi simulizi.

(iv)Kuendeleza/kuhimiza matumizi ya lugha za kienyeji.

(v)Kupambana na kusumba za kikoloni.

(vi)Kuhakikisha kuwa fasihi simulizi inahifadhiwa kwa njia ya kisayansi.

(vii)Kutenga vipindi katika radio na televisheni juu ya fasihi simulizi.

(viii)Kudhamini mashindano ya muziki na maigizo. (zozote 6x1=al.6)